JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL

MISSIONARIES OF THE PRECIOUS BLOOD
P.O. Box 2010
DODOMA – TANZANIA

tel. 0766 939 536
e-mail: jmerlinisec@gmail.com
web-site: www.cppseducationtz.sc.tz

Registration N° S 4880, NECTA Exams N° S 5391

KWA MZAZI/MLEZI WA .....

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021

Uongozi wa shule unayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule ya Sekondari John Merlini mwaka 2021.

TAFADHALI USOME KWA MAKINI MAELEZO YAFUATAYO:

1. Shule ni ya mseto (wasichana na wavulana) na ni ya bweni. Inafunguliwa **tarehe 11 Jan 2021**.
2. Ada: **kwa kidato cha I ni sh. 2,000,000/=** (Milioni mbili tu). Italipwa kwa Awamu moja, mbili au tatu tu.

   AWAMU MOJA
   - Tshs 2,000,000/= Januari kabla ya kufungua shule

   AWAMU MBILI
   - Tshs 1,000,000/= Januari kabla ya kufungua shule
   - Tshs 1,000,000/= Julai kabla ya kufungua shule

   AWAMU TATU
   - Tshs 667,000/= Januari kabla ya kufungua shule
   - Tshs 667,000/= April kabla ya kufungua shule
   - Tshs 667,000/= Julai kabla ya kufungua shule
3. Malipo ya ada yafanyike katika account zifuatazo ya **NMB Bank:**
   - **JINA LA ACCOUNT: JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL**
   - **NAMBA YA ACCOUNT: 52010026469**
   - **JINA LA ACCOUNT: JOHN MERLINI SEC. SCHOOL DORMITORY**
   - **NAMBA YA ACCOUNT: 52010031122**
4. Mwanafunzi aonyeshe ***pay in slip*** ya Benki ili kupokelewa shuleni. Adai risiti ya shule.
5. **Godoro:** Linapatikana shuleni tu kwa gharama ya **Tsh 47,000=.** Mwanao atapewa godoro jipya anapowasili na ataondoka nalo anapomaliza shule. Kiasi hiki cha fedha kilipwe shuleni.
6. **Mahitaji:**

Sare: Suruali/Sketi ya rangi ya kaki, shati jeupe, sweta rangi damu ya mzee	Zinapatikana shuleni zenye nembo ya shule, T-shirt 16,000, shati 13,000, sweta 17,000, sketi 25,000, suruali 25,000
Truck Suit 2: 1 ya rangi nyekundu na 1 ya rangi ya bluu masai	Zinapatikana shuleni zenye nembo ya shule: bei sh. 50,000/= jumla
T shirt 2: 1 rangi nyekundu na 1 rangi ya bluu	Zinapatikana shuleni: bei sh. 32,000/= jumla
Viatu vya ngozi nyeusi, soksi nyeupe	Anunuliwe nyumbani au shuleni (Ni nafuu zaidi)
Viatu vya raba rangi nyekundu	Anunuliwe nyumbani au shuleni
Viatu vya mpira (soka)	Anunuliwe nyumbani au shuleni
BIMA ya Afya (lazima kwa kila mwanafunzi)	Kama huna, shule itatengeneza: sh. 54,000/=(NHIF)
DOCASSA exams(Dodoma Catholic Sch Ass)	Tshs. 30,000/= alipe shuleni.
Kuprint majina kwenye nguo za mtoto	6,000/=
Nakala ya Cheti cha kuzaliwa	
Counter Books (Q 2) 13, Kalamu 2, Penseli 2, Kifuto1, Mathematics set 1, Madaftari madogo 13, Rula 1,	
4 figure Mathematical Tables, Concise Swahili – English Dictionary	
Rimu 2 za karatasi A4 za kukabidhi ofisini	
Ndoo, fagio, mop	
Vifaa vya usafi binafsi: sabuni ya kuogea, ya kufulia, dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka	
Kaptula na fulana kwa michezo na kazi	Sandals
Mashuka 2 rangi ya pink kwa wasichana	Kanga na kitenge kwa wasichana
Mashuka 2 rangi ya bluu kwa wavulana	Nguo za ndani
Chandarua, mto, taulo	Kiwi nyeusi
Begi la madaftari, Saa ya mkononi, trunk ya chuma	mwamvuli
NGUO ZOTE ZITAANDIKWA JINA LA MWANAFUNZI SHULENI KWA GHARAMA YA SH. 6,000/=	

NB. KUTAKUWA NA KIKAO CHA WAZAZI/WALEZI TAREHE 23.01.2021 KUANZIA SAA 3:00 ASUBUHI.

7. MWONGOZO KWA MWANAFUNZI:

a. Lengo la shule ni kumpatia mwanafunzi elimu bora na kumjenga kitabia na maadili ambayo yatamwezesha awe raia mwema. Naye mwanafunzi anatakiwa kuweka masomo mbele na kufuata kiaminifu sheria za shule na za bweni ambazo zitamsaidia kufikia mafanikio mazuri na malengo ya shule.
b. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza tu.
c. Kutolipa au kuchelewa kulipa ada kwa wakati unaotakiwa kutasababisha kusimamishwa au kuachishwa shule au kunyimwa kufanya mtihani.
d. Maktaba ya shule ina vitabu vya kutosha, lakini havitoki nje ya Maktaba. Wazazi/walezi wamnunulie mtoto wao vitabu vyake binafsi vya kujisomea.
e. Mabweni yanafungwa asubuhi saa 1:00 na kufunguliwa tena saa 10:30 jioni. Mwanafunzi akitoka bwenini asubuhi kwenda darasani awe amechukua vifaa vyote anavyohitaji kwa siku hiyo. Hataruhusiwa kurudi bwenini wakati wa masomo.
f. Siku zisizo za shule (Jumamosi mchana, Jumapili na siku zingine za sikukuu) wanafunzi watapewa nafasi ya kujihusisha na shughuli tofauti kama vile Debating clubs, Theatre, Talents show, Sports, Seminar, nk. Dhumuni ni kumpa kila mwanafunzi uwezo wa kukuza na kuweka hadharani karama zake.
g. Mwanafunzi anajukumu la kufanya usafi kila siku shuleni na bwenini katika muda unaotolewa.
h. Vifaa vya shule na vya bweni vipo katika ubora. Atakayeviharibu atagharamia utengenezaji wake.
i. Mazingira ya shule na ya bweni daima yawe ya utulivu. Kuzurura nje ya darasa, kupiga kelele, kujihusisha na shughuli zisizo za kishule hakuruhusiwi.
j. Mgeni haruhusiwi kuingia katika vyumba vya kulala wanafunzi bali anakaribishwa mahali anapooneshwa.
k. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani wakati wowote wa Muhula wa masomo isipokuwa kwasababu maalumu. Ruhusa inatolewa na Mkuu wa shule tu.
l. Kila asubuhi na jioni wote kwa pamoja watasali Sala ya asubuhi na jioni. Kila Jumapili wote watahudhuria Ibada ya Kikristu (Kikatoliki) inayoadhimishwa katika ukumbi wa shule.
m. Mwanafunzi akabidhi fedha zake binafsi kwa **Padre Hillary Ngowi.** Yeye atampatia kila anapohitaji. Uongozi wa shule hautawajibika juu ya upotevu wa fedha ambayo hakukabidhiwa Padre.
n. Mzazi/Mlezi anayemtumia hela mtoto wake kwa sababu yoyote atume kwa kupitia Padre Hillary Ngowi.
o. Mzazi/Mlezi daima adai risiti ya shule kwa fedha zote ambazo analipia shuleni na alipe kwa wahusika tu ambao ni **Mkuu wa shule na Padre Hillary Ngowi.**

8. MWENENDO WA MWANAFUNZI

Jarida linaloitwa STUDENTS HANDBOOK 2018 linaonyesha wazi taratibu zote ambazo zinamwongoza mwanafunzi akiwa shuleni na bwenini.

Hizi zifuatazo ni baadhi ya taratibu:

a. ***"Mtendee mwenzako kama unavyopenda kutendewa wewe"*** Maneno haya ya Yesu ni mzizi wa uelewa wa J. Merlini, inayowataka wanafunzi kupendana, kuheshimiana na kuthaminiana.
b. Mwanafunzi awe na adabu njema ndani na nje ya shule, mkweli, mtiifu na mwenye heshima kwa walimu, patron/matron, wafanyakazi na wanafunzi wenzake. Apokee maelekezo na maagizo yanayotolewa bila ubishi.
c. Aonyeshe moyo mwema wa kuwasaidia wanafunzi wenzake wasio na uwezo sawa na yeye. Afuate kauli mbiu ya shule inayosema: **"EDUCATION FOR SERVICE IN SOLIDARITY".**
d. **Ajitenge na makosa yafuatayo:** ugomvi wa kupigana, lugha ya matusi au ya kutisha, wizi au uharibifu wa mali ya shule na ya wengine, udanganyifu, unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, uhusiano wa kimapenzi, kumpa mimba, kupata mimba, kutoa au kushiriki kutoa mimba, kumiliki na kutumia madawa ya kulevya, kutoka nje ya eneo la shule na bweni bila ruhusa, **kuiba mitihani**.
e. Haruhusiwi kuwa na simu wala redio. Akihitaji kupiga au kupigiwa simu na wazazi/walezi itatumika simu ya shule. Kwa jumla taarifa kutoka nyumbani zinatolewa kwa kupitia Uongozi wa shule na sio kwa mwanafunzi husika moja kwa moja.
f. Sare ya kubana au fupi hairuhusiwi. Asivae urembo wa aina yoyote.

Ili shule iweze kufikia malengo yake ya kitaaluma na kinidhamu, uwepo ushirikiano mzuri kati ya Uongozi wa shule , walimu, wazazi/walezi, wafanyakazi na wanafunzi.